Local Government Reform Programme
Programu ya Uboreshaji Serikali za Mitaa

Kilimani Road
P.O. Box 3021
Dar-es-Salaam
Tel: (225 22) 666524
Lgrtz@raha.com

Kiongozi cha Mkufunzi

Mwongozo Rahisi

MBINU ZA UKAGUZI WA UMASIKINI KATIKA SERIKALI ZA MITAA



UAPP- Urban Authorities Partnership Programme
Mradi wa Ushirikiano na Mamlaka za Miji

Dar-es-Salaam City Council Building
First Floor
P.O. Box 3446
Dar-es-Salaam
Tel: (225 22) 2126243
uappdsm@africaonline.co.tz

Sura ya
1

Utangulizi

Kiongozi cha Mkufunzi: Mbinu za Ukaguzi wa Umasikini

Uzoefu wa Wakufunzi

Makala hii ya kiongozi cha Mkufunzi cha Mbinu za Ukaguzi wa Umasikini ni mkusanyiko wa mada zilizotolewa katika mafunzo ya Sekretariat za Mikoa ya Tanzania Bara katika vituo vya mafunzo vya:

1) Mwanza (12-16 Januari 2004) : Mwanza, Shinyanga, Mara, Kagera, Tabora na Kigoma.

2) Moshi (19-23 Januari 2004) : Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Singida, Dodoma, Tanga na Pwani

3) Iringa (26-30 Januari 2004) : Iringa, Mbeya, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Rukwa, Morogoro na Dar-es-Salaam

Kijitabu hiki kimetolewa kitumike na wawezeshaji toka Sekretariat za Mikoa katika kuzifundisha Halmashauri za Wilaya/Miji mbinu za ukaguzi wa Umasikini. Kijitabu hiki kitumike pamoja na kitabu kilichotolewa hapo awali chenye jina lifuatalo:

"Auditing Poverty in Tanzania a joint approach at Local Government level"

Mwongozo Rahisi

Kijitabu hiki kimerahisisha mwongozo wa awali wa mafunzo ya Mbinu za Ukaguzi wa Umasikini kama ifuatavyo:

1) Kuelezea mchakato wa mafunzo

2) Kuelezea kanuni za msingi za ufundishaji na uwezeshaji wa watu wazima

3) Kuorodhesha mada kuu au mada za msingi katika mafunzo ya Mbinu za Ukaguzi wa Umasikini

4) Kutoa tafsiri ya awali ya madodoso na miongozo ya kukusanyia taarifa na takwimu

5) Kuboresha madodoso, majedwali na zana nyingine za kutambua na kuchambua taarifa za Ukaguzi wa Umasikini

Matumizi ya Kiongozi wa Mkufunzi

- Kijitabu kinatoa mwelekeo wa jumla wa kuendesha mafunzo ya Mbinu za Ukaguzi wa Umasikini. Wawezeshaji wanaweza kuutumia mwongo huu kuandaa miongozo yao wenyewe kufuatana na mazingira halisi ya kujifunzia katika Halmashauri zao. Tafsiri zilizotolewa hapa pia zinaweza kuboreshwa ili kuifanya lugha ya uwezeshaji kuwa bora zaidi na ya kueleweka katika eneo husika.

- Mifano iliyo katika maigizo, vipindi ya kisa mkasa na chemsha bongo inaweza kutumika kama ilivyo au kuboreshwa zaidi ili kuongeza upeo wa washirki kuelewa mada husika.

Mifano ya kisa mkasa, chemsha bongo na vibwagizo ipo katika viambatanisho

Washirki na wachangiaji

Wawezeshaji wafuatao wamechangia katika kuboresha kijitabu hiki cha mwongozo wa kufundishia:

1) Washiriki wa mafunzo ya Sekretariat za Mikoa yote 21 ya Tanzania Bara

2) Wawezeshaji toka Halmashauri ya Mji Singida: A. Mujuni, Dr. Wiliam Mafwere, J. Mnyambi na Hilda Mselle.

3) Wawezeshaji toka Manisapaa ya Mbeya : Rose Matovu, na Mwl. Ngonyani.

4) Wawezeshaji toka ngazi ya Taifa: Howard Clegg wa LGRP na Josephine Lemoyan wa UAPP DSM

Sura ya
2

Mchakato wa Mafunzo

Masuala ya Kuzingatia

Mbinu na Kanuni za msingi za Mafunzo

Walengwa wa mafunzo haya ni wataalamu mbali mbali kutoka katika Halmashauri za Wilaya na Miji. Mafunzo haya yanatolewa kwao ili kuwapatia mbinu, stadi na taarifa kuhusu dhana ya Ukaguzi wa Umasikini. Baada ya Mafunzo haya washirki watawezesha utekelezaji wa ukaguzi wa umasikini katika Halmashauri zao.

Mpangilio wa Mada

Kitabu cha "Auditing Poverty Audit a Joint Approach at Local Government Level" kimeweka kwa mtiririko mada za masomo mbali mbali kuanzia sura ya kwanza hadi sura ya sita. Mwongozo huu umeongezea mada chache ili kutoa fursa kwa matukio mengine yanayohusia na mafunzo. Kwa ufupi mada zimeorodheshwa kama ifuatavyo:

1. Utangulizi wa Mafunzo

- Kujiandikisha (Karatasi, fomu au dafatari la uandikishaji lililoandaliwa)
- Kugawa vifaa (kalamu, dafatari n.k.)
- Kujitambulisha (Zoezi lililoandaliwa)
- Ufunguzi (Mgeni Rasmi)
- Matarajio ya washiriki (zoezi la vikundi)
- Sheria za Mafunzo/Warsha zinazotekelezeka zipangwe na kuwekwa wazi

2. Mbinu na Kanuni za Mafunzo

Lengo la kila mada/somo

- Lengo la kila mada/somo liwekwe wazi katika karatasi/ubao
- Mwezeshaji aandae vifaa vya kufundishia na kujifunzia kabla ya mada/somo
- Muda wa mada/somo uwekwe bayana
- Mchakato wa kutoa mada au kuwasilisha somo uelezewe
  - Maelezo toka kwa mwezeshaji
  - Kazi za washiriki (field, role plays, bunga bongo, kisa mkasa, majadiliano ya vikundi n.k.)
- Maoni ya washiriki/mwezeshaji kuhusu mada/somo husika

3. **Mbinu za Uwezeshaji wa watu wazima na matumizi yake kwenye ukaguzi wa Umasikini**

- Mbinu za Uwezeshaji
- Mbinu Maalum
- Misingi ya Ushiriki wa Jamii

4. **Ukaguzi wa umasikini**

- Maana ya Ukaguzi wa Umasikini (Zoezi katika vikundi)
- Historia fupi ya Ukaguzi wa Umasikini (Nadharia na mhadhara)
- Uhusiano kati ya mbinu za Ukaguzi wa Umasikini na mifumo inayotumia mbinu shirikishi (k.m. O&OD, PRA, na Mifumo mingine ya kupanga mipango) (Nadharia, Mhadhara na Maswali na Majibu)
- Vipengele vikuu vya Mbinu ya Ukaguzi wa Umasikini (Nadharia, Maswali na Majibu)
- Hitimisho: maoni ya washiriki na mwezeshaji

5. **Vipengele Muhimu vya PPP**

- Maelezo kuhusu PPP
- Madodoso ya PPP
- Mbinu za kutekeleza PPP

6. **Vipengele Muhimu vya PGP**

- Maelezo kuhusu PGP
- Madodoso ya PGP
- Mbinu za kutekeleza PGP
- Matumizi ya taarifa za PGP

7. **Vipengele Muhimu vya WSP**

- Maelezo kuhusu WSP
- Jedwali la WSP
- Ujazaji wa WSP
- Matumizi ya takwimu za WSP

8. **Utayarishaji wa taarifa ya Kata//Halmashauri ya Ukaguzi wa Umasikini**

- Vipengele muhimu vya taarifa
- Uchambuzi wa taarifa za PPP, PGP na takwimu za WSP
- Matumizi ya taarifa ya Ukaguzi wa Umasikini

9. **Vipengele Muhimu vya Ajenda ya Kupunguza Umasikini (katika Kata/Halmashauri- Agenda for Poverty Reduction – APR)**

- Maelezo kuhusu APR
- Namna ya kuingiza taarifa ya Ukaguzi wa Umasikini katika APR
- Matumizi ya APR

10. Maandalizi na Utekelezaji wa zoezi la Ukaguzi wa Umasikini katika Kata/Halmashauri

- Mahitaji
- Maandalizi ya wawezeshaji
- Maandalizi ya walengwa (washiriki wa msingi katika jamii)
- Hadidu za Rejea

Sura ya 3

Maelezo ya Mada na Masomo

Mifano ya Mada/Masomo

Mada na 4 Ukaguzi wa Umasikini : Maana/Tafsiri ya Ukaguzi wa Umasikini

MADA	**Tafsiri ya Ukaguzi wa Umaskini**
MALENGO YA MADA/SOMO	1. Kuleta mawazo ya washiriki kwenye mada kuu ya mafunzo (Ukaguzi wa Umasikini) 2. Kuweka tafsiri sawia ya Ukaguzi wa Umaskini 3. Kutoa tafsiri ya umaskini kulingana PRS, NPES na sera nyingine.
VIFAA	Kitini – Mfano hai, Kisa Mkasa (uk 18 wa Auditing Poverty a Joint Approach at Local Government Level) Karatasi za ubaoni Kalamu za rangi
MUDA	Dk. 10 Zoezi la kutafsiri ukaguzi; na kutafsiri ya umasikini Dk. 5 Kuwasilisha Dk 5 Michango ya vikundi vilivyobaki Dk. 30 Mada ya Mwezeshaji (majumuisho)
NJIA ZA UWEZESHAJI	**Zoezi: Tafsiri ya Ukaguzi na tafsiri ya Umasikini** 1. Washiriki watagawanyika katika vikundi vya watu wasiozidi 10 2. Kila kikundi kitafanya mazoezi yafuatayo: a). Jadili na toa maana ya ukaguzi. b). Jadili na elezea umasikini ni nini?

	3. Kila kikundi kitawasilisha. 4. Mwezeshaji atajumuisha na kutoa ufafanuzi wa somo - Maana ya umasikini kulingana na PRS na sera nyingine -Kisa Mkasa na mifano hai

Mada na 4b Historia Fupi ya Ukaguzi wa Umasikini

MADA	**HISTORIA FUPI YA MBINU ZA UKAGUZI WA UMASIKINI**
MALENGO YA MADA/SOMO	Kuwafahamisha washiriki chimbuko la mbinu ya ukaguzi wa umaskini Kuonyesha uhusiano kati ya mbinu ya ukaguzi wa umasikini na mbinu shirikishi zilizopo Kuonyesha matumizi na manufaa ya mchakato wa ukaguzi wa umasikini
VIFAA	Vitini : Historia ya Mbinu za Ukaguzi wa Umasikini na Faida Zake. Kitini katika Kompyuta (Power Point)
MUDA	Dakika 45 hadi 60
NJIA ZA UWEZESHAJI	1 Mhadhara - RRA - PRA/PLA -PA (Katika nchi zilizoendelea na zinazoendelea) - PA Tanzania - Matumizi ya PA - Manufaa ya ukaguzi wa umasikini. - Matumizi ya mbinu za ukaguzi wa umasikini. - Ukaguzi wa umasikini na mbinu shirikishi za utafiti na upangaji wa mipango. Maswali na Majibu

MAONI	MWEZESHAJI

Mada na 5 Vipengele Muhimu vya PPP

MADA	**VIPENGELE MUHIMU VYA PPP**
MALENGO YA MADA/SOMO	Kutoa maelezo ya msingi ya PPP Kuwasilisha madodoso ya PPP Kuwasilisha mbinu za kutekeleza zoezii la PPP Kuonyesha matumizi ya taarifa za PPP
VIFAA	Dodoso la PPP (Kiswahili na kiingereza) Maswali ya Mwongozo kwa watafiti Mwongozo wa Watazamaji
MUDA	Dakika 120
NJIA ZA UWEZESHAJI	1. **Mhadhara:** Vipengele muhimu vya PPP a). Masuala ya Kiuchumi b). Masuala ya Kijamii na c). Masuala ya Utawala Bora Igizo la Utekelezaji wa zoezii la PPP (matumizi ya dodoso) 2. **Igizo** : Watafiti (3) : Jamii (10) : Watazamaji (Washiriki waliobaki) Maandalizi : - Mwezeshaji atachagua washiriki wa igizo kama walivyoorodheshwa hapo juu. - Mwezeshaji atawaelekeza watafiti maswali ya kuwauliza wanajamii - Mwezeshaji pia atawapa maelezo watazamaji vipengele muhimu vya kuzingatia wakati watafiti wakiuliza maswali kama ilivyoonyeshwa katika maoni ya mwezeshaji hapo chini.

MAONI	Maelezo ya ufafanuzi wa madodoso kama yanahitajika

Mada na 6 Vipengele Muhimu vya PGP

MADA	PGP
MALENGO YA MADA/SOMO	Kutoa maelezo kuhusu PGP Kuonyesha mbinu za kutekeleza PGP Kuonyesha matumizi ya taarifa za PGP
VIFAA	Dodoso la PGP Maswali ya Mwongozo kwa watafiti Mwongozo wa Watazamaji
MUDA	Saa 1.30 hadi saa 2
MBINU ZA UWEZESHAJI	1. Mhadhara Vipengele muhimu vya madodoso Maelezo ya ufafanuzi 2. Igizo : Watafiti (2-3) : Halmashauri (10) : Watazamaji (Waliobaki)
MAONI	

Mada na 7 Vipengele Muhimu vya WSP

MADA	**WSP**
MALENGO YA MADA/SOMO	Kuwapa washiriki zana ya kukusanya takwimu za hali ya utoaji huduma katika Kata (na kijiji). Kuwapa mbinu za kuhakiki takwimu na taarifa zinazokusanywa wakati wa PPP na PGP Kuwaonyesha washiriki matumizi ya WSP Kuwapa washiriki zana ya kupanga kata kufuatana na hali ya umasikini kulinga na hali ya utoaji huduma
VIFAA	Jedwali la WSP Maelezo ya mwezeshaji
MUDA	Saa 1
MBINU ZA UWEZESHAJI	1.Mafunzo: Vipengele muhimu vya WSP : Kupitia jedwali la WSP : Kupeleka jedwali kwa WEO kwa ajili ya ujazaji : Uhakiki wa Takwimu 2. Igizo Mgawanyo wa upendeleo wa bajeti ya Halmashauri : Madiwani : Watendaji wa Halmashauri : Watazamaji Kikao cha Full Council
MAONI	

Mada na 8 Uandaaji wa Taarifa za Ukaguzi wa Umasikini

MADA	Taarifa za Ukaguzi wa Umasikini
MALENGO	Kuelezea vipengele muhimu vya taarifa Kuonyesha namna uchambuzi wa taarifa za PPP, PGP na takwimu za WSP unavyofanyika Kuonyesha matumizi ya taarifa ya Ukaguzi wa Umasikini
VIFAA	1.Maelezo ya Somo 2. Mifano ya taarifa za Kata za Ukaguzi wa Umasikini
MUDA	Saa 1-2
MBINU ZA UWEZESHAJI	1.Mhadhara: Uchambuzi wa takwimu za PPP : Uchambuzi wa takwimu za PGP : Uchambuzi wa takwimu za WSP 2. Maswali na majibu
MAONI	

Mada na 9 : Ajenda ya Kupunguza Umasikini (Agenda for Poverty Reduction –APR)

MADA	**Ajenda ya Kupunguza Umasikini (Agenda for Poverty Reduction – APR)**
MALENGO	Kuwawezesha washiriki kuandaa Ajenda/dondoo ya kupunguza umasikini kufuatana na matokeo ya PPP, PGP na WSP Kuonyesha uhusiano kati ya Ajenda/Dondoo ya kupunguza umasikini na mipango ya Halmashauri, Kata na Vijiji Kuwawezesha washiriki kuwatambua wadau mbali mbali watakao husika na utekelezaji wa mikakati ya kupunguza umasikini.
VIFAA	Jedwali la mfano la Ajenda/ Dondoo ya Kupunguza Umasikini kutoka Mbeya Slide za mada ya ajenda Jedwali la Dondoo ya Kupunguza Umasikini
MUDA	Saa 2
MBINU ZA UWEZESHAJI	1.Mhadhara : Vipengele muhimu : Mfano wa Mbeya : Namna ya kuingiza ajenda katika mpango wa Halmashauri. 2. Kazi za vikundi: Kutengeneza APR kutokana na takwimu na taarifa za PA (PPP,PGP na WSP)
MAONI	MWEZESHAJI
	WASHIRIKI

Mada na 10: Maandalizi ya Ukaguzi wa Umasikini katika Halmashauri/Kata

MADA	**Maandalizi ya PA (kazi baada ya mafunzo**)
MALENGO	Kuwawezesha washiriki kutambua vipengele vya maandalizi • Mahitaji • Maandalizi ya wawezeshaji • Maandalizi ya walengwa (washiriki wa msingi katika jamii) • Hadidu za Rejea
VIFAA	Maelezo ya somo
MUDA	Saa 1-2
MBINU ZA UWEZESHAJI	1.Mhadhara: Maelezo : Hatua 10 za maandalizi ya PA : Mazoezi ya vikundi ya upangaji wa zoezii la ukaguzi wa umasikini katika kata/Halmashauri yao
MAONI	MWEZESHAJI
	WASHIRIKI

Mada na: 1 Kujitambulisha (Mfano wa Jedwali la Mkufunzi)

MADA	**Jina la Mada**
MALENGO YA MADA/SOMO	Unachotarajia baada ya mada/somo
VIFAA	Orodhesha vifaa vya kufundishia, kujifunzia
MUDA	Muda utakaotumika kuendesha mada/somo
MBINU ZA UWEZESHAJI	1. orodhesha mbinu za kufundishia 2. Onyesha hatua zitakazofuatwa
MAONI	WAWEZESHAJI
	WASHIRIKI

Kanuni, Zana na Njia Shirikishi za Uwezeshaji

1. Kanuni za uwezeshaji

Kuwafahamu washiriki
Punguza tofauti kati ya washiriki na mwezeshaji
Tumia lugha muafaka
Chagua eneo muafaka
Kuwapa heshima washiriki
Heshimu michango ya washiriki

2. Mbinu za Uwezeshaji (mbinu nyingine na ufafanuzi wa ziada upo hapo chini na katika vimbatanisho mbali mbali katika mwongozo huu)

Majadialiano
Usaili
Majadiliano ya vikundi
Bunga bongo
Kisa Mkasa

3. Mbinu Maalum

Uchunguzi kwa kuangalia (observation)
Usaili (Interviews)
Matumizi ya zana za kalenda na mstari wa wakati (calendars and time lines)
Matumizi ya ramani (Maps)
Orodha na awekaji wa vipaumbele (Ranking, priority setting)
Mrejesho na uhakiki (feedback and verification)

4. Misingi ya ushiriki wa Jamii

Kwanza: Watu ni msingi

Pili: Thamini ufahamu na mbinu walizokuwanazo wanajamii

Tatu: Ushiriki wa jamii huzingatia kuwajasirishaji wa wanawake

Nne: Uhuru wa mawazo

Tano: Taratibu na maamuzi ya jamii hujibu matatizo ya kijamii

Sita: Fursa kwa watu kujiamualia njia za utatuzi wa matatizo yanayowakabili na kubuni njia za utekelezaji

5. Manufaa ya ushiriki wa jamii

Kwanza: Ushiriki dhabiti wa wadau (Stakeholder commitment)

Pili: Njia bora ya kuwafikia walengwa (Improved targeting)

Tatu: Kupata takwimu za uhakika (More realistic data)

Nne: Huboresha mbinu za kufikia muafaka (Improved negotiating skills)

Tano: Gharama nafuu (Cost reduction)

Sita: Huongeza uendelevu (Enhanced sustainability)

6. Zana mbali mbali za PRA zinazotumika Ukaguzi wa Umasikini.

PRA ni mkusanyiko wa stadi, mbinu na njia shirikishi zinazowawezesha watu kutoa mawazo yao
na kuchambua hali ya maisha ya kila siku na jinsi fursa au vikwazo mbali mbali huathiri maisha yao
ya kila siku. Kwa kutumia mbinu na njia hizo shirikishi, watu huweza kujiamulia namna ya kutatua
matatizo yao kwa kujiwekea mipango, mikakati ya utekelezaji, na utaratibu wa kutathimini na
kupima matokeo ya juhudi zao.

Ni njia iliyotokana na mbinu ya RRA (Rapid Rural Appraisa). Tofauti kati ya RRA na PRA ni kwamba PRA inasisitiza mchakato wa kuwawezesha wana jamii kuwa na mtazamo wa kujitatulia matatizo yao kwa njia na raslimali zilizo ndani ya jamii yao wenyewe. PRA huwapatia watu ujasiri wa kupambana na makali ya maisha na kujiletea maendeleo yao. Lakini RRA ilikuwa ni mbinu ya wataalamu kutoka nje ya jamii wanaoifikia jamii kwa ajili ya kukusanya takwimu na taarifa ili zikatumike kwa ajili ya masuala ya maendeleo.

PRA hutumia njia mbali mbali za kuwawezesha wanajamii kutoa mawazo yao, kuchangia katika mijadala, kutoa taarifa na kusaidia katika uchambuzi wa taarifa zinazokusanywa. Njia nyingi za PRA ni za vitendo, hushirikisha watu mbali mbali kutoa majibu kwa njia za vitendo zinazoonekana wazi wazi

Njia na zana za PRA

- Ramani(Maps): huonyesha makazi ya watu na maeneo yenye raslimali mbali mbali k.m. maji, misitu, vituo vya kutolea huduma, barabara, mapito ya wanyamapori n.k.

- Michoro (flow diagrams): huonyesha mtiririko wa mahusiano ya matukio na masuala mengine ya kijamii. Husaidia kutambua na kuchambua visababisho vya matukio mbali mbali, matokeo ya matukio hayo, matatizo na njia za utatuzi.

- Kalenda za misimu (seasonal calendars): huonyesha upatikanaji wa chakula, mgawanyo na mzigo wa kazi katika kaya, hali ya lishe na afya katika kaya, bei, kipato na masuala mengine yanayobadilika katika misimu mbali mbali ya mwaka.

- Majedwali (matrices or grids): hutumia njia na vifaa rahisi kama vile mbegu, mawe na hata vijiti ili kulinganisha vitu, raslimali n.k. Zana hii hutumika kuonyesha thamani ya vitu tofauti kama vile mazao, miti n.k. na hali ya mabadiliko katika jamii

Historia ya Mbinu ya Ukaguzi wa Umasikini

- Kabla ya miaka ya 80 watafiti walitumia fedha nyingi na muda mrefu kufanya utafiti katika jamii
- Mbinu za ukusanyaji taarifa na takwimu zilikuwa za kuwanufaisha watafiti na wataalamu.
- Wataalamu walibuni njia bora zaidi za kukusanya taarifa na takwimu katika jamii.
- Njia iliyobuniwa ilikuwa ni RRA (Rapid Rural Appraisal) ambayo ilikuwa na upungufu ufuatao:
    - Wataalamu walichukuwa takwimu na kuondoka bila kutoa mrejesho
    - Mbinu hii ilikuwa pia ina na tabia ya kutoa maelekezo toka juu kwenda chini.
    - Haikuwa na sifa ya kujenga uwezo na
    - Ushiriki wa wanajamii ulibaki kuwa hafifu
- katikati ya miaka ya 80 mbinu ya RRA iliboreshwa.
- PRA na PLA ni mbunu zilizofuata baada ya kuboresha RRA.
- PRA ilikuwa ni mkusanyiko wa njia shirikishi za kukusanya taarifa na kuandaa mipango shirikishi ya jamii.
- PLA ni mkusanyiko wa njia shirikishi za uwezeshaji.
- PPA ni moja kati ya mbinu za kutathmini hali ya Umasikini katika jamii kwa kutumia njia shirikishi.
- PPA ilitumika nchini Tanzania huko Shinyanga kupima hali ya umasikini.
- Ukaguzi wa umasikini hutumika katika nchi mbali mbali duniani kutathmini hali ya umasikini. Lakini mbinu zilizokuwepo kabla ya hii zilikuwa na upungufu kwani hazikuwa na kipengele cha utawala bora.
- Mbinu ya Serikali za Mitaa ya Ukaguzi wa Umasikini yaani Poverty Audit (PA) ni mbinu ya kitaifa inayotekelezwa kupitia LGRP kwa uwezeshaji wa UAPP na Halmashauri shiriki za Manispaa ya Mbeya, H/Miji ya Mtwara Mikindani na Singida.
- Mbinu hii ilibuniwa mwaka 2001, na kufanyiwa majaribio katika Manispaa ya Mbeya mwaka 2002.
- Mbinu ya ukaguzi wa umasikini iliboreshwa mwaka huo huo kwa ushirikiano na wawakilishi kutoka Sekretariat za Mikoa ya Mwanza, Mtwara, Pwani Morogoro na Dar-es-Salaam, LGRP, TAMISEMI na wawakilishi toka UNDP na REPOA.
- Baada ya warsha iliyotajwa hapo juu, Halmashauri za Miji ya Mtwara Mikindani na Singida kwa uwezeshaji wa mradi wa UAPP zilitumia mbinu hizi na kujumuisha matokeo ukaguzi wa umasikini katika mipango ya maendeleo na ya utoaji wa huduma ya Halmashauri zao.
- Mbinu hii ni ya kipekee na imebuniwa na kuboreshwa hapa Tanzania.
- Mbinu hii hutumika kuchambua sera na mipango ya utoaji wa huduma hivyo kuna nafasi kubwa ya kuboresha sera na mipango ya kuondoa umaskini katika ngazi zote.
- Tofauti kati ya PA na PPA ni:
    - Kipengele cha ukaguzi wa utawala bora hakipo katika PPA

    - PPA ina upungufu katika kutathmini ugumu (complexity) wa hali ya umasikini
    - PPA haina hatua ya kuandaa mkakati wa kupunguza umasikini.
    - Hakuna mlinganisho wa takwimu za utoaji huduma katika kata kwa ajili ya kutambua kata zenye hali duni na masuala mengine yanayohusu umasikini.
    - PPA haina kipengele cha uchambuzi wa sera za kuondoa umasikini.
- PA ni mbinu inayowawezesha wanajamii wenyewe kutafiti, kuchambua na kupima matokeo ya taratibu za maisha yao wenyewe.
- PA hutilia mkazo kujenga uwezo wa jamii na kutoa nafasi ya kutoa maamuzi.

PA SI O BLUE PRINT Inaweza kuboreshwa zaidi na watumiaji.

Mada na 4 b. Tafsiri na sifa za Mbinu ya Ukaguzi wa Umasikini

UKAGUZI WA UMASIKINI NI NINI?:

Ukaguzi wa umasikini ni muhimu kwa sababu hali ya umaskini katika jamii huathiriwa na sera, mikakati, programu, miradi na bajeti, utoaji wa ruzuku na misaada, namna sera za kitaifa zinavyotekelezwa katika ngazi zote

Ukaguzi wa umasikini ni mchakato unaotumika na serikali za mitaa, kwa kushirikiana na wadau wengine kutathmini sera, mipango, bajeti na miradi ili kutambua kama ina mtazamo wa kuondoa umasikini

Ukaguzi wa umasikini hupima utekelezaji halisi wa mikakati ya kuondoa umasikini katika jamii

Ukaguzi wa umasikini huchambua sababu za umasikini na matokeo ya hali ya umasikini katika jamii

Ukaguzi wa umasikini unaangalia ni kwa jinsi gani raslimali za umma zinavyotumika kuboresha maisha ya watu masikini

Ukaguzi wa umasikini haushindani wala kufuta taratibu zilizopo za kuandaa mipango ya maendeleo.

Huboresha sera, utendaji katika ngazi ya jamii na pia hutumika kujenga hoja ya madhubuti ya kubadili mipango ya kitaifa ili iwe na mwelekeo wa kupunguza umasikini

Huchunguza na kukagua sera mipango ya kisekta, na bajeti katika ngazi za serikali za mitaa ili kuhakikisha kawamb malengo ya kitaifa ya kupunguza umasikini yamezingatiwa.

Mada na 4c Uhusiano wa Ukaguzi wa Umasikini na Sera, programu mifumo ya Kitaifa na mbinu nyingine shirikishi

Dira ya Taifa (Vision 20 25): Lengo kuondoa umasikini

TAS: Tanzania Assistance Strategy: Ina lengo la kuondoa umasikini

PRS: Mkakati wa Taifa wa Kupunguza umasikini

LGRP: Lengo kuu ni kupunguza umaskini

MDG: Ina lengo la Kupunguza Umaskini uliokithiri na njaa (Eradicate extreme poverty and hunger).

Mifumo: MTEF
PRA
O&OD



Mada na 5: Vipengele Vikuu vya Mbinu ya Ukaguzi wa Umasikini

(PPP, PGP WSP Na Agenda for Poverty Reduction APR)

PPP : Participatory Poverty Profiling

- Inakusanya taarifa kutoka kwa watu wa kawaida
- Taarifa hizi ni mtazamo na hisia za watu kuhusu masuala ya
  - Kiuchumi
  - Kijamii
  - Kisiasa
- PPP huchambua namana masuala haya yanvyoathiri maisha yao na kuchangia katika hali ya umasikini ndani ya jamii

- Hutumia njia shirikishi za utafiti.
- Mwongozo wa kukusanyia Habari umeandaliwa

PPP Hutueleza makundi ya watu wa kawaida wanasema nini

PGP: Policy and Governance Profile

- Inakusanya taarifa kutoka kwa madiwani, kiongozi mkuu wa Halmashauri na wakuu wa idara.
- Taarifa zinazokusanywa ni sera zinazohusu umaskini, utawala , taratibu za kisheria za kuendesha Halmashauri, na mali za maskini .

- Hutumia dodoso lililotayarishwa maalum

PGP hutueleza watendaji na watunga sera wanasema nini

WSP : Ward Statistical Profile

- Inakusanya takwimu kutoka ofisi za Kata na Vijiji
- Wahusika wa kutoa takwimu hizi ni Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji
- Takwimu zinazokusanywa ni zile zinazohusu takwimu za wakazi, ajira na takwimu za hali ya utoaji huduma katika Kata.
- Hutumia jedwali lililoandaliwa

WSP hutuonyesha takwimu mbalimbali kuhusu hali ya upatikanaji wa huduma za kijamii katika Kata.

APR : Agenda for Poverty Reduction (Ajenda ya Kupunguza Umasikini

- Ajenda ya kupunguza umasikini ni mkusanyiko wa masuala muhimu yaliyoibuliwa na PPP,PGP na WSP
- Masuala haya huandaliwa mapendekezo ya ufumbuzi katika ngazi ya kijiji, kata na Halmashauri.
- Ajenda ya kupunguza umasikini katika ngazi ya Halmashauri hutoa mapendekezo ya ufumbuzi yanayoingizwa katika mpango wa mwaka mmoja na mpango wa miaka 3 wa Halmashauri.

Zoezi kwa washiriki

Mwezeshaji awaulize washiriki kama wanaweza kivielezea vipengele vikuu vya mbinu ya Ukaguzi wa Umasikini vilivyoonyeshwa katika jedwali lililotajwa



Faida za Ukaguzi wa Umasikini

Husaidia kudhihirisha wazi tatizo la umaskini.

- Huonyesha wazi wazi mgawanyo usio sawia wa raslimali na huduma na jamii
- Huwezesha watu masikini kujua mategemeo yao
- Huwawezesha watendaji kutambua umuhimu wa kuwianisha sera na utekelezaji

Hukuza uelewa wa masuala ya umasikini

- Huwawezesha watu maskini kuelezea mahitaji yao na namna mahitaji hayo yanavyoweza kupatikana
- Huonyesha jinsi aina mbali mbali za umasikini zinavyohitaji ufumbuzi tofauti
- Huonyesha jinsi aina mbali mbali za umasikini zinavyohitaji matumizi tofauti tofauti ya fedha/bajeti

Huimarisha Utawala Bora

- Huwajibisha watendaji watoe huduma kwa ufanisi na haki
- Huweka wazi uhusiano kati ya sera na utekelezaji.

Huimarisha utekelezaji wa Sera za nchi katika ngazi ya jamii

- Huonyesha uhusiano kati ya sera za kitaifa na matokeo yake katika ngazi ya jamii
- Hurahisisha kuboresha au kubadilisha sera za kitaifa wakati wa maandalizi na utekelezaji wake

Huimarisha ushirikiano kati ya wadau mbali mbali

- Hutoa fursa kwa watendaji wa Serikali za Mitaa, wahisani, na wawakilishi wa asasi za kiraia kukutana na watu masikini
- Hutoa fursa kwa watu maskini kuchangia katika mchakato wa kutunga sera

Hujenga Utamaduni wa kushirikiana

- Hutoa fursa ya mikutano kati ya wahisani na vikundi mbali mbali vya kijamii
- Hujenga imani kati ya makundi mbali mbali na ushiriki wa jamii katika kupanga kutekeleza kusimamia na kuthmini miradi mbali mbali

Hujenga Umiliki wa mipango

- Hutumia habari na takwimu zilizopo ndani ya jamii kuandaa mipango.
- Ushirikiano na jamii huwezesha raslimali za ziada kupatikana

Mada na 5 a. Igizo la Matumizi ya Dodoso la PPP

IGIZO : Mwongozo wa watafiti

Watafiti 3

Watafiti watawaandaa wanajamii waliochaguliwa kwa ajili ya usaili.
Watafiti wataendesha zoezi lao kufuatana na maswali yaliyoandaliwa.
Watafiti wataandika majibu katika flip chart ili washiriki na watazamaji waweze
kuona matokeo ya usaili.

Mwongozo wa watazamaji:

1.Uwezeshaji

- Je mwezeshaji anatumia mbinu za uwezeshaji
- Mkao wa washiriki ukoje?

2. Elezea uulizaji wa maswali- je wanauliza maswali kwa kuzingatia dodoso?

- Je maswali ya nyongeza anayouliza mwezeshaji ni muafaka?

3. Chunguza na elezea tabia na mtazamo wa mwezeshaji

4. Je wanajamii wanaelewa maswali?

5. Elezea mtazamo wa wanajamii kwa mwezeshaji

Mada na 5 c. Dodoso la Kiswahili la PPP

PPP – Muhtasari wa Maswali, Mada, na Njia za Uwezeshaji

Masuala ya Kiuchumi	**Maswali**	**Njia na Maelezo**
Umaskini na Mbinu za Kujikimu		
Tafsiri za umaskini na mbinu za kujikimu	1(a)-2(b), 6(d)	PRA/PPA n.k.
Historia na sababu za umasikini	3(a)-3(d)	Matukio ya Kihistoria Mstari wa nyakati
Umasikini wa Kudumu	4	Majadiliano ya vikundi na tafiti
Maeneo wanapokaa watu maskini	5	PRA/ramani/Majadilia no katika vikundi
Mahitaji, Matatizo na Umasikini	6(a)-(6c)	PRA/majadiliano katika vikundi /Uwekaji wa vipaumbele
Fursa za Kiuchumi		
Vyanzo vya Mapato na fursa za kiuchumi	7-9	Majadiliano katika vikundi / Usaili
Uzalishaji wa mazao ya kilimo na uwezo wa kifedha	10(a)-10(d)	Majadiliano katika vikundi / Usaili
Mikakati ya kujikimu	11(a)-(11b)	Majadiliano katika vikundi
Huduma na Ustawi wa Jamii		
Hali ya utoaji wa huduma na ustawi wa jamii	12(a)-12(g)	Majadiliano katika vikundi / Usaili /Uchunguzi

Masuala ya Kijamii	Maswali	Njia na Maelezo
Mila na Desturi		
Migogoro ya kijamii, Imani na njia za utatuzi	13(a)-13(e)	Majadiliano katika vikundi
Taasisi na Umaskini		
Taasisi na njia za kupunguza umasikini	14-17	Majadiliano, Uwekaji wa vipaumbele, Chapati na uchunguzi
Jinsia na Uwakilishi		
Ushiriki wa jamii katika siasa	28	Majadiliano katika vikundi
Fursa za Upatikanaji wa raslimali na huduma	29- 30(b)	Majadiliano katika vikundi

Masuala ya Utawala Bora	Maswali	Njia na Maelezo
Umaskini na Utawala Bora		
Ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za umma	18(a)- 8(d)	Majadiliano katika vikundi
Mipango na bajeti shirikishi	19(a) –21	Majadiliano katika vikundi
Mrengo wa Umasikini	22-24	Majadiliano katika vikundi
Uwajibikaji na Demokrasia		
Uwazi na mjadala	25(a)-26	Majadiliano katika vikundi
Udhibiti na Utatuzi wa migogoro	27(a)-27(c)	Majadiliano katika vikundi
Umasikini na Masula ya Uhakika wa chakula		
Hali dhalili, uhakika wa chakula na mikakati ya kujikimu	31(a)- 33	Majadiliano katika vikundi , Matukio ya kihistoria na kalenda za kujikimu

Mada na 5 d Dodoso la PPP

Masuala ya Kiuchumi

Umasikini na hali ya maisha	
1a	Orodhesha makundi ya watu kulingana na uwezo wao kiuchumi katika jamii
1b	Elezea sifa za kila kundi
2a	Nini kinahitajika ili kumbadilisha mtu masikini kuwa tajiri?
2b	Nini kinahitajika ili ?
3a	Eleza historia ya umasikini katika eneo hili hadi sasa
3b	Nini chanzo/sababu za umasikini katika eneo hili?
3c	Je, kuna kipindi maalumu katika mwaka ambacho watu wanapata umasikini?
3d	Je, ni watu hao hao kwa kila mwaka?
4	Je, ni vigezo vipi vinawafanya baadhi ya watu kuwa masikini wa kudumu?
5a	Je, kuna sehemu yoyote katika kijiji/mtaa/kata ambako masikini wanaishi?
5b	Ni kwa nini wanaishi sehemu hiyo?
6a	Ni yapi matatizo makuu ya kifamilia (yapange 1 – 5 kwa umuhimu)
6b	Ni yapi matatizo makuu ya kijamii (yapange 1 – 5 kwa umuhimu5)
6c	Je, matatizo haya yana uhusiano wowote na umasikini? Eleza
6d	Ungekuwa na fursa kubadilisha kitu kimoja cha kuboresha maisha yako, ungependelea kitu gani?
Fursa za Kiuchumi	
7	Orodhesha vyanzo vikuu vya mapato
8	Orodhesha fursa za kiuchumi zilizopo katika eneo lako
9	Ni vikwazo gani vinavyozuia matumizi ya fursa zilizotajwa hapo juu
10a	Je, uzalishaji wa mazao ya biashara unaongezeka au unapungua?
10b	Je, uzalishaji wa mazao ya chakula unaongezeka au unapungua?
10c	Je, mapato yatokanayo na mazao yanakuwezesha sasa kununua mahitaji yako kwa wingi zaidi ukilinganisha na miaka mitano iliyopita?
10d	Je, uzalishaji wa mifugo unaongezeka au unapungua?
11a	Je, wakati wa hali mbaya ya uchumi familia (kaya) masikini zinakabilianaje na hali hiyo?
11b	Je, familia masikini zinaweza kukopa, bidhaa na zana za kazi? Kama ndiyo kutoka kwa nani na kwa kiwango gani cha riba?
Huduma za Kijamii	
12a	Je, huduma za elimu zimeboreka au ni mbaya zaidi katika kipindi cha miaka 5 iliyopita? Kwa vipi?
12b	Je, huduma za afya zimeboreka au ni mbaya zaidi katika kipindi cha miaka 5 iliyopita? Kwa vipi?

12c	Je, barabara zimeboreka au ni mbaya zaidi katika kipindi cha miaka 5 iliyopita? Kwa vipi?
12d	Je, huduma za maji zimeboreka au ni mbaya zaidi katika kipindi cha miaka 5 iliyopita? Kwa vipi?
12e	Je, taratibu za kupata ardhi sasa zimeboreka au zimezidi kuwa ngumu katika kipindi cha miaka 5 iliyopita? Kwa vipi?
12f	Je, huduma za ugani kama vile kilimo, mifugo, maendeleo ya jamii na misitu zimeboreka au zimedorora kwa kipindi cha miaka 5 iliyopita? Kwa vipi?
12g	Je, nyumba za bati zimeongezeka kwa kipindi cha miaka 5 iliyopita?

… inaendelea ukurasa unaofuata …

… Kutoka ukurasa uliopita …

Dodoso la PPP

Masuala ya Kijamii	
Mila na Desturi	
13a	Kuna migogoro gani mikuu katika jamii?
13b	Nini vyanzo vya migogoro hiyo?
13c	Je, migogoro hii husababisha umasikini
13d	Ni imani na mila zipi zinazochangia kuwepo umasikini katika jamii
13e	Je, kuna taratibu gani za kijamii zinazokwamisha ujasirimali (ubunifu wa kimaendeleo)?
Asasi na Umasikini	
14	Je, ni Taasisi/Asasi gani zilizoko katika kijiji/mtaa
15	Je, ni Taasisi zipi zenye mahusiano ya karibu zaidi na wakazi wa kijiji/mtaa/kata
16	Je, kati ya Taasisi hizo ni zipi una imani nazo zaidi (kwa kiwango gani? Juu, kati, chini)
17	Je, ni Taasisi zipi zenye uwezo zaidi katika kuleta mabadiliko ya kiwango cha umasikini katika jamii
Jinsia na Uwakilishi	
28a	Je, wanawake kutoka katika familia masikini wanashawishiwa kujitokeza katika kugombea nafasi za uongozi katika chaguzi na/au viti maalumu katika ngazi ya kijiji?
28b	Je, wanawake kutoka katika familia masikini wanashawishiwa kjitokeza katika kugombea nafasi za uongozi katika chaguzi na/au viti maalumu katika ngazi ya kata?
28c	Je, wanawake kutoka katika familia masikini wanashawishiwa kjitokeza katika kugombea nafasi za uongozi katika chaguzi na/au viti maalumu katika ngazi ya wilaya?
29	Je, watoto wanaotoka katika familia masikini wanapata vikwazo katika kuhudhuria shule? Kama vipo vitaje
30a	Ni sababu zipi zinazopelekea/changia umasikini wa wanawake?
30b	Je, ni nani ananufaika zaidi kutokana na rasilimali na shughuli za maendeleo katika kaya? Elezea

… inaendeleao ukurasa unaofuata

… Kutoka ukurasa uliopita …

Dodoso la PPP

Masuala ya Utawala	
Umasikini na Utawala Bora	
18a	Taja idadi ya watu wanaopaswa kulipa kodi mbalimbali za halmashauri
18b	Wangapi wamelipa kodi mwaka jana?
18c	Je watu masikini wanafahamu kodi hizo zinavyotumika?
18d	Je, watu masikini wananufaika na kodi hizo? Kama ndiyo, ni manufaa yapi?
19a	Je, wananchi wanashiriki kupanga shughuli za maendeleo? Wanashirikije?
19b	Je, watu wanapata taarifa ya namna bajeti za Halmashauri zinavyotumika (ndiyo/hapana)
19c	Nani anayetoa taarifa hizo?
20	Taja vipaumbele vyako vitatu kati ya haya yafuatayo: Elimu, Afya, Maji, Kilimo, Mifugo na Barabara.
21	Kwa kiwango gani (chini, kati, juu) kwa watu masikini kuwa na fursa za kutoa mawazo kulingana na mahitaji yao kuhusu:
21a	Vipaumbele vya maendeleo ya halmashauri yao
21b	Mgawanyo wa bajeti
21c	Uchaguzi wa wawakilishi
21d	Mikataba ya halmashauri
21e	kujitegemea na kuchangia
21f	Ubora wa huduma za afya na elimu
21g	Upatikanaji wa maji
21h	Haki za kumiliki ardhi
22	Je, mipango ya halmashauri za wilaya inayafikia makundi yafuatayo:
22a	Jamii nzima (ndiyo/hapana) eleza
22b	Watu wenye uwezo (ndiyo/hapana) eleza
22c	Watu masikini sana (ndiyo/hapana) eleza
23	Je, mipango ya taasisi zisizo za kiserikali (za ndani ya nchi, za kimataifa, za kidini) inayafikia makundi yafuatayo:
23a	Jamii nzima (ndiyo/hapana) eleza
23b	Watu wenye uwezo (ndiyo/hapana) eleza
23c	Watu masikini sana (ndiyo/hapana) eleza
24	Je, iwapo fedha zitapatikana kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya watu masikini ungependelea zipitie kwa nani kati ya hawa wafuatao kwa ajili ya utekelezaji?
24a	Bajeti ya halmashauri
24b	Taasisi isiyo ya kiserikali/shirika la dini
24c	Kamati ya maendeleo ya kata
24d	Kamati ya maendeleo ya kijiji

… inaendeleao ukurasa unaofuata …

… Kutoka ukurasa uliopita …

Dodoso la PPP

Uwajibikaji na Demokrasia	
25a	Je, serikali ya kijiji/kata inakutana mara kwa mara?
25b	Kikao cha mwisho kilifanyika lini?
25c	Je, mkutano mkuu wa kijiji unaitishwa/unafanyika kwa mujibu wa sheria?
25d	Mkutano mkuu wa kijiji wa mwisho ulifanyika lini?
25e	Je, Madiwani hukutana mara kwa mara na wapiga kura wake (ndiyo/hapana)
25f	Mikutano hiyo inahusu nini?
25g	Mkutano wa mwisho ulifanyika lini?
26	Je, wananchi wanapata taarifa za wakati wa kufanyika kwa mkutano wa baraza la madiwani na wanaelewa kuwa wana uhuru wa kuhudhuria? Eleza
27a	Je, wananchi wako huru kulalamika dhidi ya matendo ya ubadhilifu yanapojitokeza?
27b	Je, wananchi wanatumia njia gani kutoa malalamiko yao dhidi ya vitendo vya ubadhilifu?
27c	Je, malalamiko hya yanshughulikiwa vipi ndani ya jamii?
Umasikini na uhakika wa Chakula	
31a	Je, namna gani wananchi masikini wanapata chakula wakati wa njaa?
31b	Ni nani mwingine anayesaidia kupunguza tatizo la njaa?
32	Ni matukio yapi ya majanga na yasiyotabirika yaliyoisha tokea tangu mwaka 1997?
33	Ni nini matokeo ya matukio yaliyo orodheshwa hapo juu, kuhusu hali ya uhakika wa chakula katika kaya masikini?

Mada na 5 e Kisa Mkasa: Mfano kutokana na Matumizi ya PPP

Mfano– Mtazamo wa watu kuhusu umasikini Katika Halmashauri ya Mtwara/ Mikindani

Masikini sana

- Mtu aliyekata tamaa
- Hawezi kutosheleza mahitaji yake ya msingi k.v. chakula, mavazina makazi.
- Anategemea wengine wampe chochote ni omba omba
- Hachagui ajira atafanya kazi yeyote aweze kupata mradi wake.
- Hana mwanzo wala mwisho hajui la kufanya
- Hamiliki ardhi au raslimali nyingine yeyote
- Hupata mlo mmoja tu kwa siku
- Kipato chake hakikidhi mahitaji ya msingi
- Mgonjwa mwenye uwezo mdogo wa kufikiri
- Mjinga haujui kusoma wala kuandika
- Hana ajira wala hajajiajiri
- Jamii wala ndugu hawamtegemei
- Ni rahisi kufa pakitokea tatizo lolote

Mfano – Kisa Mkasa cha Sofia Pesatatu (Mjane)

Sofia Pesatatu ni mama wa watoto watatu. Anatokea kijiji cha Mahuta katika wilaya ya Newala. Ana umri wa mika 33. Kwa sasa Sofia anaishi katika Kata ya Vigaeni Ward Halmashauri ya Mji wa Mtwara/Mikindani. Sofia aliolewa na Alli Sumaku, amabaye ni mfanyabiasha mwaka 1984. Waliishi mjini Dar es Salaam. Katika kipindi cha ndoa yao, walifanikiwa kujipatia mali zifuatazo:

- Kiwanja kwa ajili ya makazi huko Kurasini, Dar es Salaam
- Shamba na nyumba huko Nanyamba, Mtwara Vijijini
- Vifaa vya nyumbani

Mnamo mwaka 1987 mume wa Sofia alifariki dunia kutokana na ajali ya gari huko Dar es Salaam. Marehemu aliacha mtoto mmoja. Baada ya tukio hilo ilibidi Sofia arudi kwao Mtwara ili kuishi na wakwe zake. Katika muda wa mwezi mmoja mali na vifaa vya mume wake viligawiwa kwa ndugu za marehemu bila yeye mwenyewe kufahamu wala kutoa kauli yeyote. Kutokana na tatizo hili la mirathi na matatizo mengine yaliyozuka baada ya kifo cha mume wake, Sofia aliamua kurudi kwa wazazi wake huko Mahuta Newala.

Mwaka 1988 Sofia aliolewa tena na mfanya biashara wa Newala na walihamia mjini Mtwara. Walifanikiwa vile vile kujipatia mali kama vile cherehani, na vifaa vingine. Sofia alibahatika kupata watoto wawili Kwa bahati mbaya mumewe wa pili pia laifariki dunia mwaka 2000.

Kwa sasa Sofia anaishi na watoto wake watatu wenye umri wa miaka kati ya 8 na 12. Watoto wote wanasoma na Sofia anafanya biashara ndogo ndogo ili kujikimu. Sofia alielezea mkasa wake kwa uchungu mkubwa huku akikubali kuwa yote yametokana na mapenzi ya Mungu.

Huu ni mfano wa mjane mmoja kati ya wajane wengi katika jamii waliodhulumiwa haki na kunyanyaswa na ndugu za waume zao.

Maskini

- Hana huduma nyingine yeyote zaidi ya chakula, mavazi na makazi
- Mara nyingi yupo katika matatizo.
- Anamudu kuwapatia watoto elimu ya msingi
- Hapati msaada wowote.
- Ana watoto wengi
- Elimu yake ni ndogo/duni
- Mlevi
- Ana uwezo wa kufanya kazi lakini hana vitendea kazi, wala raslimali
- Ni mzururaji
- Ni bahati kwake kupata milo mitatu kwa siku.
- Hana uhakika wa maisha yake kwa siku zinazokuja
- Anamiliki nyumba chakavu
- Anamiliki ardhi kidogo kwa ajili ya mazao ya chakula. Mazo hayaridhishi
- Mwenye kipato cha familia kubwa
- Huduma za msingi anazopata haziridhishi

Mada na 6 Igizo la PGP: Uwajibikaji na Utawala Bora- Majibu Hewa na Taarifa za Nadharia

Mwongozo wa Igizo la PGP

Washiriki wa Igizo

Mkurugenzi, Mwenyekiti wa Halmashauri, Madiwani na Wakuu wa Idara (6)
Wawezeshaji/Watafiti (2)

Maswali ya Wawezeshaji

1. Mtafiti 1: Je unazifahamu sera za nchi zinazoelekeza kupunguza umasikini?
2. Mkurugenzi: Ndiyo. Tunazifahamu sera hizi. Na tumeazimia kununua magari mapya matano L/C VX kwa ajili ya kuwafikia walengwa.
3. Mtafiti 1: Je HoD anaifahamu sera ya Idara ya Kilimo? Ndiyo. Tumeanzisha huduma za ughani za kulipia.
4. Mtafiti 2: Samahani hata mimi sina nakala, je nitaweza kupata kutoka kwako?

5. Mtafiti 1: Je lengo la kupunguza umaskini limeunganishwa katika Dira ya Halmashauri na malengo na madhumuni ya Halmashauri?
6. Mkurugenzi : Ndiyo
7. Mtafiti wa 2 : Ndugu Mkurugenzi sijui nitaweza kuzipata maana hapa ukutani zsizioni
8. Mkurugenzi: Mchumi hebu tupatie nadhani tuliziandaa katika mpango wetu wa 2002
9. Mtafiti 2: Tafadhali naomba nifafanulie mgawanyo wa bajeti ya halmashauri katika kata zenu
10. Madiwani: Mgawanyo hutegemea uwezo wa kata katika kuchangia “Mwenye kisu kikali ndiye mla nyama”
11. Mtafiti na 1 : Je kuna hali yoyote ya upendeleo katika ajira ndani za Halmashauri
12. Madiwani: Hapana ajira zote zinafuata utaratibu wa kutangaza na kuhudhuria usaili

Mada na 6: Dodoso la PGP

Dodoso la PGP na Maelezo

Sera ya Umasikini		
Maswali		**Maelezo ya Mwongozo na Uhakiki**
1	Je, Baraza la halmashauri ikijumuisha watendaji na madiwani wa naelewa wera za Taifa za upunguzaji wa umasikini kama zilivyoelezwa katika mpango wa Taifa wa kuondoa umasikini na mpango wa kuboresha serikali za mitaa.	Kagua na hakikisha kama madiwani na watendaji wana nakala za Kiswahili za PRSP, LGRP, TAS and Dira 2025, NPES
2	Kuna juhudi zozote zilizofanyika kujumuisha sera hizo katika mipango na bajeti katika ngazi ya halmashauri	
3	Kwa namna gani upunguzaji umasikini unajidhihirisha katika dira, mwelekeo na malengo ya halmashauri	Pitia taarifa na nyaraka husika
4	Je, miongozo ya kitaifa inayohusiana na upunguzaji umasikini inatekelezwa na halmashauri?	Dhibitisha kwa kupitia mihutasari ya vikao vya Halmashauri, mipango na vipaumbele vya wakazi
5	Ni kwa kiwango gani mapungufu ya vigezo vya kitaifa vya utoaji huduma vinatumiwa kama vigezo vya ugawaji rasilimali?	Hakikisha kama madiwani na watendaji wanfahamu viwango vya utoaji huduma (national standards of service delivery). Onyesha viwango vya utekelezaji na visharia vya utoaji huduma kama inawezekana
6a	Kila kata ugawiwa asilimia ngapi ya bajeti ya halmashauri?	
6b	Asilimia 30 ya kata zilizoainishwa na wilaya kuwa masikini zaidi zinapata sehemu gani katika bajeti ya maendeleo na makusanyo ya halmashauri	Inafikiriwa kwamba taswira ya hali ya umasiki katika Halmashauri inaonyesha hali ya umasikini katika kata kwa kuziorodhesha kata kufuatana na hali ya umasikini. Chunguza mgawanyo wa bajeti katika kata kwa kuzingatia mgawanyo wa matumizi ya bajeti (kwaida na maendeleo). Zoezi hili litaonyesha kiwango cha mgawanyo wa bajeti katika kata. Linganisha mgawanyo unaolekezwa katika asilimia 30 za kata maskini zaidi
7	Kwa kiwango gani maslahi ya watu masikini zaidi katika jamii yanawasilishwa katika kamati ya fedha na mipango ya halmashauri,	Kamati za kudumu za Halmashauri zina uwezo wa kuwaalika washiriki toka katika taasisi mbali mbali za kijamii na watu maarufu katika mikutano ya kwa ajili ya

	ikiwa ni moja kwa moja au kupitia uwakilishi wa vikundi vya kijamii?	kupata michango yao. Kutokana na fursa hii, taasisi na vikundi vinavyowakilisha masikini na walio katika mazingira magumu vinaweza kualikwa katika mikutano ya kamati hizi
8	Je, halmashauri ya wilaya imeweka malengo yanayohusu kaya masikini zaidi au kaya zote bila kujali viwango vya mapato yao? Kama jibu ni ndiyo, kwa vipi?	
9a	Je, ni kwa namna gani utaratibu wa kuchangia gharama unahakikisha kwamba familia masikini hazinyimwi kupata huduma muhimu za msingi?	Nia ya swali hili ni kuhakikisha kuwa kaya masikini sababu za msingi hazina uwezo wa kuchangia kwa hali na mali katika shughuli za maendeleo hazitengwi bali zinanufaika na matokeo ya shughuli za maendeleo na huduma mbali mbali za kijamii. K.m. Iwapo wazee na yatima hawana uwezo wa kuchangia katika ujenzi wa darasa au kituo cha afya, wawekewe utaratibu maalum ili wao pia wanufaike na huduma za elimu na afya.
9b	Je, kuna taratibu gani zilizopo za kuwathibiti watoa huduma wa umma na binafsi?	Taratibu za “Safety nets” ni njia/mkakati wa kuwalinda watu masikini wasitumbukie katika hali ya umasikini uliokithiri. Taratibu hizi ni k.v. e.g. “Mfuko wa elimu” katika ngazi zote
Utawala Bora		
Maswali		**Maelezo ya Mwongozo na Uhakiki**
10	Je, halmashauri ya wilaya/miji/manispaa/jiji inatangaza kuwepo kwa mikutano yake mapema na iko wazi kwa jamii?	Halmashauri zinawajibika kutangaza mikutano yake katika muda muafaka kwani wananchi wana haki ya kuhudhuria vikao vinayowahusu. Vile vile wananchi wana haki ya kutoa maoni yao ili wawakilishi wao wayapeleke katika vikao husika. Baada ya usaili, wawezeshaji wanahitajika kuhakikisha kama ratiba za mikutano zipo na zimewekwa bayana kuwawezesha wananchi kujua tarehe za mikutano.
11	Je, halmashauri au kamati zake ndogo zinashauriana na wadau wakuu wanaoguswa na sera na hasa wadau waliosahaulika kijamii na kiuchumi?	Angalia maelezo ya swali la 5 hapo juu. Pia iwapo uamuzi wa halmashauri unamwelekeo wa kuathiri kikundi au eneo fulkani, ni vizuri kuwashirikisha na kujadiliana na wadau wote athari za uamuzi unaotarajiwa.
12	Je, kumbukumbu za makusanyo ya halmashauri huwekwa wazi? Idadi ya vitabu vilivyotolewa na kurudishwa, kiasi kilichokusanywa na kilichobakia kijijini/katani/mtaa, pamoja na maoni kutoka katika taarifa ya mkaguzi	Upo ushahidi kwamba rushwa imekithiri katika nyanja ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri hasa kodi ya maendeleo. Mataizo yanayojitokeza mara kwa mara na yanayosababisha upotevu wa fedha ni pamoja na kupotea kwa vitabu vya kukusanyia

	mkuu wa mahesabu ya serikali kuhusu makusanyo ya mapato katika wilaya.	mapato, kuwepo kwa vitabu visivyo halali sambamba na vile vya Halmashauri, kutokuwepo kwa nakala rasmi na utata kati ya fedha zilizowasilishwa na zile zilizokatiwa stakabadhi, na, kutokuwepo uthibitisho wa malipo kwatika vitabu husika. Mara nyingi, taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali imeonyesha upungufu katika ukusanyaji wa mapato ya serikali hasa kutoka katika chanzo cha kodi ya maendeleo. Ni vizuri kutumia taarifa hizo wakati wa uhakikiki.
13	Je, kuna uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa zabuni wa kazi za umma na usimamizi wa ubora katika utekelezaji	Hakiki kwa kutumia taarifa za mikutano ya bodi za tenda na taarifa za utendaji kutoka ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa. Fanya majadiliano na wazabuni mbali mbali ili kupata maoni yao juu ya taratibu za zabuni.
14	Je, utaratibu wa utoaji wa posho kwa madiwani na watendaji unawiana na vyanzo vya mapato ya halmashauri?	Hakiki kiwango cha bajeti ya Halmashauri kilichotengwa kwa ajili ya masurufu na posho mbali mbali. Linganisha uwiano wa posho na bajeti kwa ujumla Hakiki iwapo mfumo wa masurufu/posho ni wazi kwa wote (full council)
15	Je, ni njia ipi rasmi ya mawasiliano inayotumika kati ya madiwani/kata/vijiji/mitaa kuhusiana na sera za halmashauri na maamuzi ya utekelezaji?	Ni muhimu kuhakikisha kama upo mfumo wa upelekaji wa taarifa na habari na uwajibikaji kwa raia
16	Je, upendeleo ni hatari katika ajira ndani ya halmashauri? Je, kanuni zilizopo za ajira za TUMITAA zinatoa nafasi sawa ya ajira kwa wote wakiwemo wanawake na wasio wenyeji?	Ni kosa kubagua kwa namna yeyote ile (kwa misingi ya kabila, jinsia, dini, ulemavu n.k.) katika taratibu za ajira. Hii imeelezwa katika kanuni za TUMITAA. Hivyo upendeleo wakati wa ajira hauruhusiwi. Ajira hutolewa kwa misingi ya elimu na uzoefu. Ili kuhakiki kama taratibu zilizokubalika za ajira zinatekelezwa ni vyema kufuatilia taarifa za kamati ya ajira na kuchambua utendaji wa kamati katika miaka 2 iliyopita.Taratibu za TUMITAA zitumike kuongoza uhakiki huo. Ikiwezekana waajiriwa watarajiwa wanaweza kufanyiwa usaili
17	Je, mfumo wa sasa wa hesabu za fedha za serikali, (platinum) unatoa nafasi kwa jamii kuchambua ufanisi wa matumizi ya fedha?	Ili mfumo wa uwekaji taarifa za hesabu za Halmashauri (IFMS) itumike ipasavyo ni lazima kumbu kumbu za hesabu ziingizwe kila siku. Vile vile ni muhimu kuwa na mweka kumbukumbu aliyefuzu. Iwapo vipengele hivi havitatimizwa, utaratibu wa kuweka kumbukumbu kwa kutumia mfumo

		wa kuaandika kwa mkono unaweza kutumika. Ni muhimu kuangalia kama kompyuta zilizopo zinafanya kazi vizuri na upatikanaji wa umeme ni wa kuaminika kwani mara nyingi umeme ni tatizo katika Halamshauri nyingi. Swali la msini hapa kwa ajili ya kuhakiki taarifa zinazotolewa ni kupata tarehe ya mwisho ya kuingizia kumbu kumbu za fedha katika kompyuta. Angalia mfumo upi ni wa masingi katika Halmashauri. Ule wa kompyuta (IFMS) au ule wa wa kutumia vitabu vya kuandika kwa mkono (manual system)
18	Je, halmashauri zinashirikisha mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na Asasi mbalimbali katika mikutano na utekelezaji wa shughuli zake?	Utafiti umeonyesha kwamba shughuli za Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGO's) zimnaelekezwa kwa jamiii masikini kwa ufanisi zaidi kuliko zile za Halmashauri (Serikali). Kwa hiyo, ushirikiano kati Halmashauri, vyama vya kiraia na mashiriki yasiyo ya kiserikali utawezesha kuboresha hali ya masiha ya watu masikini. Halmashauri itanufaika iwapo itaandaa mazingira mazuri ya kuziwezesha taasisi na asisi mbali mbali kutekeleza shughuli zao. Kimsingi, shughuli nyingi za taasisi hizi huandaliwa kufuatana na vipaumbele vya kupunguza umasikini kama vile vitakavyojitokeza katika ajenda ya kupunguza umasikini na zile zinazojitolkeza mara kwa mara katika taarifa za Halmashauri. Uwakilishi wa asisi zisizokuwa za kiserikali katika mikutano muafaka ya Halmashauri ni jambo la msingi katika utekelezaji wa kanuni ya uwajibikaji
19	Je, vijiji/mitaa vinahimizwa kumiliki mipango/miradi yao kupitia misaada ya wachangiaji mfano taratibu za hatua kwa hatua na kujitegemea	Hakikisha taarifa kwa kupitia taarifa za bajeti na mgawanyo wa fedha za maendeleo katika vijiji/kata. Mapango shirikishi wa vijiji unaowaunganisha wadau mbali mbali na Halmashauri ni lazima uendelezwe (tumia mifano toka katika kijitabu cha madaraka vijijini 1975)

Kanuni za Halmashauri

Maswali		**Maelezo ya Mwongozo na Uhakiki**
20	Ukichukua kata masikini zaidi wilayani, je hali ya barabara ikoje wakati (a) msimu wa mvua} – Kutoka	Fuatilia kwa kutembelea maeneo husika. Hakiki kwa kutumia takwimu za mfumo wa SM wa Ufuatiliaji na Tathmini "the Local Government Monitoring and Evaluation (LG M+E) system".

	kwenye vitongoji (b) kiangazi} kwenda vijijiini, sokoni na maeneo mengine ya huduma za jamii	
21a	Je, maafisa wa ugani wa halmashauri wanatembelea maeneo wanakoishi watu masikini mara kwa mara?	
21b	Kwa wastani ni mara ngapi watumishi wa ughani wanatembele maeneo ya wakazi masikini au wenye mazingira magumu?	Hakiki utaratibu wa safari za watumishi ughani katika rejesta / kitabu cha wageni katika ofisi za WDC na Serikali za vijiji (viutabu katika ofisi za WEO na VEO)
21c	Kuna vituo vingapi vya kutolea huduma katika maeneo wanayokaa watu masikini	
22	Je, ushuru wa bidhaa unafuatana na wingi wa bidhaa zinazouzwa?	Angalia orodha ya viwango vya ushuru wa masoko
23a	Je, nafasi za kazi zimeongezeka kwenye kata masikini? Nafasi ngapi?	Hakikisha taarifa kupita ofisi ya mipango/mchumi, Idara ya Elimu (kitengo cha vijana), kitengo cha Ushirika na Idara ya Maendeleo ya Jamii
23b	Je, ni watu wangapi wanaishi katika maeneo masikini wameweza kujiajiri wenyewe katika kipindi cha mwaka 1 uliopita?	
23c	Je, ni watu wangapi wameweza kupata ajira baada ya mafunzo ya ufundi staid (vocational training) katika kata masikini?	
23d	Je, ni biashara ngapi zimeanzishwa katika kata masikini mwaka uliopita?	
24a	Je, halmashauri zina mpango shirikishi wa kuondoa umasikini ulioandaliwa kikata kwa kushirikisha asasi za jamii?	Rejea maelezo ya swali la 18
\24b	Mpango ulitekelezwa vipi na umepata mafanikio yapi?	
24c	Mpango huu unachangia vipi katika kuboresha huduma za kijamii na kiuchumi, pamoja na kujenga uchumi imara na endelevu.	

25	Je, kilimo ngazi ya kijiji, kina uhaba wa nguvu kazi? Kama ndiyo, kwa nini?	
26a	Shughuli za kilimo na utoaji huduma mbalimbali zimeathirika vipi kutokana na tatizo la ugonjwa wa UKIMWI (AIDS)?	Hakikisha habari kupitia Idara ya Afya, Mratibu wa Ukimwi wa Wilaya na Afisa Utumishi
26b	Je, suala la jinsia na umri linahusiana vipi na tatizo la ukimwi?	
26c	Je, mipango sahihi ya elimu ya ukimwi ipo katika kila idara za halmashauri?	
Rasilimali ya Masikini		
Maswali		**Maelezo ya Mwongozo na Uhakiki**
27	Je, halmashauri inatoa kinga ya kisheria ya kuhakikisha umiliki wa ardhi kwa ajili ya makazi na shughuli za kilimo, vijijini na mijini? Je, madai ya ardhi yanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria?	Hakikisha kupitia idara ya ardhi
28	Je, kuna mkakati wa kitamaduni unaoshirikisha wananchi katika kulinda/kuhifadhi mila na desturi; imani, elimu, ngoma za kiasili, kazi za bega kwa bega na mshikamano wa kijamii.	Wasiliana na Idara ya Elimu, Utamadiuni na Vijana kuhakiki taarifa utakazopata. Kutokana na mlipuko wa mila za kigeni, soko huria na utandawazi, kuna hatari ya kufifilisha mila na taritibu nzuri za asili. Ni muhimu kuendeleza mila, ngoma, tungo, semi za asili ili kuhakikisha kuwa urithi huu unaendelezwa kwa ajili ya kizazi kijacho.
29	Je, kuna sheria ndogo ndogo za kudhibiti na kusimamia matumizi bora ya ardhi, maji na maeneo ya malisho.	Hakiki taarifa unazopata kupitia Ofisi ya Mwanasheria wa Halmashauri, Idara ya ardhi, maliasili na mipango miji.

Mada na 7b: Jedwali la Takwimu za Utoaji Huduma katika Kata (WSP)

Jedwali la Takwimu za Huduma katika Kata

Takwimu za wakazi	Wanaume		Wanawake		Jumla	
	Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
Jumla ya Wakazi						
Watoto chini ya miaka 15						
Watu wenye umri wa kuanzia miaka 55						
Watu masikini						
Watu masikini sana						
Walipa kodi						

Elimu	
Idadi ya shule za msingi	
Idadi ya watoto walitorajiwa kuandikishwa 2004	
Idadi ya watoto walioandikishwa darasa la kwanza 2004	
Idadi ya shule za Sekondari (za serikali)	
Idadi ya shule za Sekondari (binafsi)	
% nafasi wazi za waalimu	
% ya waalimu wa daraja “A”	
% wakazi wasiojua kusoma na kuandika	
% ya waliofaulu darasa la nne	
%ya walioaulu darasa la saba	
Nett enrolment rate	
Kiwango cha utoro (drop out rate)	
Uwiano wa wanafunzi kwa darasa	
Iuwiano wa wanafunzi kwa mwalimu	
Uwiano wa vitabu kwa mwanafunzi	
Uwiano ya wanafunzi kwa madawati	
% ya wanafunzi waliofaulu darasa la VII lakini wameshindwa kujiunga na kidato cha I	
Gross primary school enrolment rate	
Kiwango cha wasicha /wavulana katika shule za msingi	
% of cohort completing standard VII	
Kiwango cha waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza	
% ya wanafunzi waliofaulu shule ya masingi kwa alama/daraja A	
% ya wanafunzi waliofaulu shule ya masingi kwa alama /daraja B	
% ya wanafunzi waliofaulu shule ya masingi kwa alama /daraja C	
Idadi ya mashimo ya vyoo kwa wasichana	
Idadi ya mashimo ya vyoo kwa wavulana	
Idadi ya wanafunzi wenye ulemavu - Wasioona	
Idadi ya wanafunzi wenye ulemavu - Wasiosikia/wasiosema	
Idadi ya wanafunzi wenye ulemavu - Ulemavu wa viungo	
Idadi ya wanafunzi Albino	

Afya	
Idadi ya vituo vya afya	
Idadi ya zahanati	
Idadi ya wakazi wanaohudumiwa na zahanati muja (wakazi/zahanati)	
km za mraba kwa zahanati (sq. per dispensary)	
% ya wagonjwa wa	
Kuhara	
HIV/AIDS	
Malaria	
TB	
Homa ya manjano	
Idadi ya wafanya kazi wa afya	
% ya nafasi wazi za kazi	

Kilimo	
Ekari za kilimo cha mazao ya chakula kwa kaya	
Ekari za kilimo cha mazao ya biashara kwa kaya	
% ya wanaotumia mbolea za viwandani	
% ya wanaotumia aina nyingine za mbolea	
% ya mazao yanayouzwa	
Umbali (Km) toka shambani hadi kwenye soko	
Idadi ya watumishi wa Idara ya kilimo	
% nafasi wazi za Kilimo	

Ajira	
Idadi ya wakazi walioajiriwa	
% idadi ya watu katika sekta ya kilimo (wakulima)	
% ya watu katika ajira ya sekta nyingine	
% ya watu katika sekta isiyo rasmi	
Idadi ya vibarua wahamiaji	
Idadi ya wanawake katika sekata isiyo rasmi	

Maji na Usafi wa Mazingira	
Idadi ya vituo vya maji	
% kaya zenye mabomba ya maji	
% kaya zenye vyoo	
Wastani wa umbali hadi kwenye kituo cha maji	
% ya wagonjwa wa magonjwa yanatokanayo na maji	
Idadi ya watumishi wa Idara ya Maji na usafi wa mazingira	
\% nafasi wazi za idara ya maji na usafi wa mazingira	

Mada na 9: Ajenda ya Kupunguza Umasikini : Agenda for Poverty Reduction

Slide 1

AGENDA YA KUPUNGUZA UMASIKINI KATIKA ENEO SHIRIKISHI

Slide 2

MAANA YA AGENDA YA UMASIKINI

- AGENDA YA KUPUNGUZA UMASIKINI NI NYENZO AMBAYO INAJUMLISHA MATOKEO YA TAARIFA ZA UTAFITI KUTOKA KWENYE MADODOSO YA PPP, PGP NA JEDWALI LA WSP.
- AGENDA YA UMASIKINI INABAINI MASUALA MUHIMU YALIYOJITOKEZA (***MAIN ISSUES)*** NA KUYAHUSISHA NA UTATUZI UNAOTARAJIWA KUFANYIKA NA WAHUSIKA MBALIMBALI KATIKA UTEKELEZAJI.

Slide 3

- **PPP** - NINI MAWAZO YA WATU WA KAWAIDA
- **PGP** - NINI MAWAZO YA WATAALAMU NA WATUNGA SERA
- **WSP** - TAKWIMU ZINAONYESHA NINI

Slide 4



Slide 5

JINSI YA KUANDAA AJENDA YA UMASIKINI KWA KUTUMIA JEDWALI

1. UPATE MAKUBALIANO KUHUSU MASUALA MUHIMU (***MAIN ISUES***) KUTOKA KWA WADAU KATIKA ENEO SHIRIKISHI. MASUALA HAYA YASIZIDI SITA. UNASHAURIWA KUYACHUKUA MASUALA HAYA KUTOKA KWENYE MADA KUU ZA DODOSO LA LA PPP.

Slide 6

2. KWA KILA SUALA MUHUMU UPATE MAKUBALIANO KUHUSU MATATIZO SUGU AU MATATIZO MAKUBWA (***CONCRETE PROBLEMS)*** YALIYOBAINISHWA KWENYE PPP, PGP NA WSP.
3. KWA KILA TATIZO KUBWA)(CONCRETE PROBLEM) TAJA UTATUZI WA KIUFUNDI (***TECHNICAL SOLUTION)*** KWA UJUMLA. HILI LITAKUWA NDIYO LENGO AMBALO LITATAFIKIWA KATIKA MIPANGO YA UTEKELEZAJI YA BAADAYE

Slide 7

4. KWA KILA UTATUZI WA KIUFUNDI TOA MAELEZO MAFUPI YA YA AINA YA SHUGHULI (ACTION) ITAKAYOFANYIKA ILI KUTATUA TATIZO LILOPO.
5. UNAWEZA KUONYESHA UMUHIMU WA UTEKELEZAJI WA KILA SHUGHULI KWA KUONYESHA KWENYE JEDWALI KATIKA SEHEMU YA LINI/MUDA (***TIME***) KWA KUONYESHA KAMA SHUGHULI HIYO ITAFANYIKA KATIKA KIPINDI CHA MUDA MFUPI (***IMMEDIATE***), MUDA WA KATI (***MEDIUM)*** NA MUDAMREFU (***LONG TERM).***

Slide 8

- 6. KWA SABABU SHUGHULI HAZIWEZI KUFANYIKA ZENYEWE, HIVYO ONYESHA KATIKA JEDWALI SEHEMU YA MUHUSIKA (***AGENCY)*** NI NANI ATAKAYETEKELEZA SHUGHULI HIYO, KAMA VILE HALMASHAURI, WAHISANI, ASASI MBALIMBALI PAMOJA NA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI (NGOS)

Slide 9

- ***KUMBUKA KUWA UBONGO WA BINADAMU UNASOTA KUWA NA ZAIDI YA MAWAZO SABA KWA WAKATI MMOJA. KWA HIYO KAMA UNAYO ORODHA YA SHUGHULI ZAIDI YA SABA TAFUTA SABABU YA KUGAWA SHUGHULI HZO KWENYE ORODHA MBILI***

Slide 10

NGAZI ZA AJENDA YA UMASIKINI

- AJENDA YA UMASIKINI INAWEZA KUTAYARISHWA KATIKA NGAZI YA WILAYA, KATA NA KIJIJI. KATIKA HALI HALISI, AJENDA YA UMASIKINI INAZINGATIA MAWAZO KUTOKA KATIKA AJENDA ZA UMASIKINI ZA KATA NA VIJIJI

Slide 11

- IKUMBUKWE KUWA AjENDA YA UMASIKINI HAIFIKII KIWANGO CHA KUTAYARISHA BAJETI AU KUANDAA RATIBA YA UTEKELEZAJI (ACTION PLAN). KAZI HII INAACHIWA HALMASHAURI YENYEWE AU MUHUSIKA YEYOTE ATAKAYEFANYA UTEKELEZAJI

Slide 12

- IKUMBUKWE KUWA HATUHITAJI KUANDAA MCHANGANUO WA KINA KWA SABABU HATUNA FEDHA WALA WATU WA KUTOSHA ILI KUWEZA KUTATUA MATATIZO YOTE YALIYOBAINISHWA KWA MARA MOJA. KWA HIYO, ILI KUFANIKISHA ZOEZI HILI TUNATAKIWA KUFUATA HATUA ZIFUATAZO.

Slide 13

1. KWANZA ANDAA AJENDA ZA JUMLA KWA KUTUMIA
   a. ***TAARIFA NYINGI IWEZEKANAVYO***
   b. ***YAANGALIE MATATIZO KWA MTAZAMO WA WADAU WENGI IWEZEKANAVYO***

Slide 14

- ORODHESHA MASUALA MUHIMU NA MATATIZO YALIYOJITOKEZA. WADAU WAWEKE VIPAUMBELE VYA MASUALA YALIYOTAMBULIWA BAADA YA KUJADILIANA NA KUKUBALIANA KWA PAMOJA.

Slide 15

3. HATIMAYE, ANDAA RASIMU YA MPANGO MKAKATI NA UISAMBAZE KWA IDADI KUBWA YA WADAU KWA AJILI YA KUPATA MAWAZO YAO AU KUPATA NYONGEZA KUTOKA KWAO PAMOJA NA WAO KUFANYA MAREKEBISHO KWENYE RASIMU PALE INAPOFAA.

Slide 16

- IKUMBUKWE KUWA AJENDA YA UMASIKINI NI MCHAKATO AMBAO UNAANGALIA MASUALA MUHIMU AMBAYO YANAPATIKANA KATIKA MPANGO MKAKATI WA MIAKA MITATU WA HALMASHAURI, PAMOJA NA MPANGO WAKE WA MUDA WA MWAKA MMOJA

Slide 17

- AJENDA YA UMASIKINI INALENGA KATIKA KUBORESHA MICHAKATO MBALIMBALI ILIYOPO NA SIYO KUWA MBADALA WA MICHAKATO HIYO

Slide 18

JEDWALI LA AJENDA YA UMASIKINI

Suala Muhimu	**Tatizo sugu**	**Ufumbuzi wa kiufundi**	**Hatua**	**Muda**	**Muhusika**
Utawala Bora	Ushiriki mdogo wa Jamii	Kuboresha Uyshiriki wa Jamii katika kuandaa Mipango	Kuwezesha jamii katika kuandaa mipango shirikishi	Katika muda mfupi	Halmashauri NGOs Wahisani

Slide 19



Mada na 10: Maandalizi ya Ukaguzi wa Umasikini katika Halmashauri/Kata

Zoezi la ukaguzi wa umasikini ni mchakato wa kukusanya takwimu za PPP, PGP na WSP na baadaye kuunganisha takwimu na taarifa hizo katika taarifa ya kata au Halmashauri ya ukaguzi wa umasikini

Zoezi hili linahitaji maandali kwani linahitaji mchango wa hali na mali kutoka kwa wadau mbali mbali wa masuala ya maendeleo katika kata na Halmashauri. Lifuatalo ni jedwali linalotuonyesha kwa ujumla ni hatua gani zifuatwe ili kutekeleza zoezii hili. Tafadhali zingatia kwamba hatua hizi zinaweza kuboreshwa kufuatana na hali halisi ilivyo katika kata au Halmashauri husika.

Hatua Kuu	**Hatua Ndogo ndogo**
Maandalizi	1. Kuanzisha kamati ndogo ya kuwezesha shughuli ya Ukaguzi wa Umasikini katika Halmashauri 2. Kuwatambua washiriki na wadau wa zoezi la ukaguzi wa Umasikini 3. Kupata msimamo wa wadau kuhusu uchangiaji na uwezeshaji wa zoezii la ukaguzi wa Umasikini (Mkutano wa Wadau) 4. Kuboresha zana za kukusanyia takwimu na taarifa mbali mbali za ukaguzi wa umasikini ikiwa ni pamoja mfumo wa taarifa ya Ukaguzi wa Umasikini 5. Kuandaa ratiba ya mikutano mbali mbali ya washiriki na watoa taarifa za Ukaguzi wa Umasikini
Taswira ya Umasikini	6. Ukusanyaji wa takwimu na taarifa (PPP,PGP na WSP) 7. Kuchambua na kuandaa taarifa za PPP, PGP na WSP na kuziunganisha kuwa taarifa moja ya Ukaguzi wa Umasikini (halamshauri /Kata)
Ajenda ya Kupunguza Umasikini	8. Kupitia taarifa za PPP, PGP na WSP ili kupata rasimu ya ajenda za kupunguza umasikini 9. Kuandaa taratibu za kuwasilisha taarifa ya ukaguzi wa umasikini na ajenda ya kupunguza umasikini kwa wadau kwa ajili ya kupata maoni na kufikia muafaka (Ajenda zinaweza kuwasilishwa katika mikutano ya wadau ili kufikia muafaka) 10. Kuandaa na kuwasilisha ajenda za kupunguza umasikini zilizokubalika na wadau Halmashauri ili ziweze kuunganishwa katika mipango ya Halmashauri /kata.

Uchambuzi na Utambuzi wa Wadau

Zoezi hili linahitaji juhudi wa pamoja na ushirikiano wa wadau mbali mbali. Sekretariat ya Mkoa ni mwezeshaji mkuu (msimamizi) katika mkoa. Fedha za Uwezeshaji zinaweza kupitia Sekretariat ya Mkoa kwenda kwenye Halmashauri husika.

Ni lazima kutekeleza mchakato wa kuwatambua wahusika wakuu wa ukaguzi wa umasikini na majukumu yao . Idadi ya wahusika na majukumu yao yatatokana na zoezii la uchambuzi. Kijisanduku kilichopo hapa kulia kinaonyesha makundi makuu ya wadau wa ukaguzi wa umasikini

Afisa mipango wa Halmashauri ni mratibu wa zoezii hili katika Halmashauri. Iwapo hana wataalamu wa kutosha anaweza kutafuta utaalamu toka nje ya Halmashauri baada ya kushauriana na Sekretariat ya Mkoa

Wadau ni watu binafsi, vikundi taasisi n.k. ambao kwa namna moja au nyingine wanataguswa na zoezii la ukaguzi wa umasikini

Wadau wa msingi Ni wale wanaoguswa moja kwa moja na watanufaika au kuathirika na zoezii hili.

Wadau wa Upili Hawa ni wawezeshaji wa kama vile wataalamu wa RS au Halmashauri watakaowezesha help to deliver the benefits.

Wadau wakuu ni wale wenye uwezo wa kuathiri na kuwezesha mafanikio ya ukaguzi wa umasikini k.v wanasiasa, watunga sera, wafadhili n.k

Mada na 10 b: Hadidu za Rejea za Utekelezaji wa Ukaguzi wa Umasikini katika Halmashauri/Kata

Halmashauri ya ……

Matumizi ya Dodoso la PPP

Vikundi Vitakavyotembelewa:

a. Wanawake (10 –15) wasio na wadhifa katika uongozi wa kata/kijiji au mtaa

b. Wanaume (10-15) – Kama hapo juu

c. Vijana (10-15) – Vijana wa kike na kiume wasio na wadhifa katika uongozi wa kata/kijiji

d. Mchanganyiko (10-15) – Wanawake na wanaume wasio na wadhifa katika uongozi wa kata/kijiji

e. Watu maarufu na viongozi (10-15) Wanawake, wanaume hata vijana walio katika uongozi au asasi za kiraia au uongozi wa kimila.

Kwa kila kikundi zingatia mambo yafuatayo:

1. Andaa utangulizi (elezea zoezi, wahusika, eneo, tarehe/muda n.k.)

2. Tumia mbinu shirikishi katika kuuliza maswali

3. Nukuu hali halisi ya mambo kama watu wanavyoeleza na mifano wanayoitoa

4. Kumbuka tafsiri ya umasikini kwa mapana yake

5. Katika kila kikwamishi, tatizo au kisababishi cha umasikini elezea jinsi wadau wanavyopendekeza kutatua. Mwezeshaji anaweza kusaidiana na washiriki kuandaa jedwali dogo la utatuzi.

6. Dhibitisha (verify) takwimu au taarifa unazopewa. Ulizia kama unaweza kupata Vidhibitisho.

7. Nukuu vyanzo vya taarifa au takwimu (k.m. VEO, WEO, watumishi ughani, kikundi kilichoshiriki n.k.)

8. Weka orodha ya washiriki: wawezeshaji na washiriki

Matumizi ya Dodoso la PGP

Washiriki: Watunga sera na wasimamizi wakuu wa utekelezaji wa sera za Halmashauri

a. Mkurugenzi wa Halmashauri

b. Wakuu wa Idara

c. Mwenyekiti wa Halmashauri

d. Waheshimiwa Madiwani

Idadi ya washiriki itategemea na maandalizi. Hata hivyo inashauriwa kuwa watendaji wakuu na watoaji
wa maamuzi ya Halmashauri ni washiriki wakuu wa PGP. Inashauriwa kuwa wawakilishi wa madiwani hasa kamati ya Fedha na Mipango/Fedha na Utawala washiriki katika zoezii hili.

Matumizi ya Jedwali la WSP

Watoa Takwimu:

Mtendaji wa Kata na timu yake ya watumishi ughani ni watoa takwimu wakuu. Watumishi ughani wanaohitajika hapa ni:

a. Mratibu wa Elimu Kata kwa ushirikiano na waalimu wakuu katikakata husika

b. Bwana/Bibi Kilimo/Mifugo wa Kata

c. Bwana/Bibi Afya wa Kata

Chemsha Bongo (Mazoezi na vibwagizo vya kuwachangamsha washiriki)

Zoezi la 1: Machungwa 5

Kuna watu 5

Na kuna machungwa 5 katika kikapu.

Kila mmoja anachukua chungwa moja.

Lakini loh! chungwa moja linabaki katika kikapu

Hali hii inawezekanaje? (wa mwisho aliondoka na kikapu kikiwa na chungwa ndani yake)

Zoezi la 2: Kukimbia na Mluzi.....

Nini kinaweza kukimbia lakini hakiwezi kutembea?
Kinapiga mluzi lakini hakiwezi kuongea? (gari moshi)

Zoezi la 3: Usinivunje!!!

Nini kitu ni rahisi sana kuvunjika hata kwa kutaja jina lake tu? (ukimya)

Zoezi la 4: Mbio----------

Nini hukimbia tu kamwe hakitembei (maji ya mto)

Zoezi la 5: Juu, Chini Daima

Nini katika kukitumia ni lazima kiende juu chini na si chini juuu? (Mwavuli)

Zoezi la 6: Mambo ya Sheria.....

Je ni inakubalika kisheria mwanamume kumuoa mjane wa dada yake?

Zoezi la 7: Zunguka

Nini kumezunguka nyumba lakini hakisogei (wigo)